BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Thelathini na Nne – Tarehe 18 Juni, 2026

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Zitasomwa.

## I. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

338. MHESHIMIWA MOHAMMED ALI SALIM (Jimbo la Ziwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

(a) Je, Serikali imefanya utafiti wa kina kuhusu ongezeko la uchafuzi wa mazingira hususani katika maeneo ya vijijini, unaochangiwa na shughuli za vijana za kujiajiri kama vile uchomaji wa mkaa, ubanguaji wa kokoto na uchimbaji wa mchanga kwa lengo la kujipatia kipato, hali inayosababisha uharibifu wa mazingira na kuchochea mabadiliko ya tabianchi.

(b) Je, ni matokeo gani ya tafiti hizo kuhusu kiwango cha athari za shughuli hizo kwa mazingira na maisha ya wananchi.

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

106. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ:

Soko la Darajani ni miongoni mwa soko kongwe sana hapa Zanzibar ambalo hivi sasa lina uwezo wa kutoa huduma zake mpaka usiku.

Hata hivyo, wafanyabiashara wanaofanya biashara nyakati za usiku, wanasumbuliwa na kufukuzwa na askari wa Malamka ya Mji Mkongwe na Idara Maalumu, jambo ambalo halileti picha nzuri.

(a) Kwa nini kusiwekwe utaratibu mzuri wa wafanyabiashara hao kujengewa meza za kuweka biashara zao badala ya kupanga chini na Serikali ikapata kodi, kuliko kuwafukuza moja kwa moja.

(b) Je, Serikali haioni muda umefika kwa soko la Darajani kufanya kazi hata saa 24, ili kutanuwa wigo wa huduma kama ilivyo kwa masoko mengine makongwe ya nchi jirani.

130. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Kwa kuwa Serikali ilikuwa na mradi wa Mji Salama ambao ulihusisha uwekaji wa kamera za ulinzi katika maeneo ya mji ili kudumisha usalama na ulinzi wa mji wetu. Na kwa kuwa hivi sasa wananchi wengi wamekuwa wakiweka wenyewe kamera za ulinzi katika maeneo yao ya makaazi, ili kudhibiti vitendo vya uhalifu na kamera hizo zimekuwa msaada mkubwa katika kubaini matukio ya uhalifu yanapotokea na kurahisisha uchukuliwaji wa hatua.

(a) Je, Serikali ipo tayari kupunguza au kuondoa kodi kwa vifaa vya ulinzi kama “CCTV” na mitambo yake, ili wananchi wengi waweze kuweka katika maeneo na kutanua wigo wa ulinzi na usalama katika mitaa yetu.

(b) Je, katika kuunga mkono uendelezaji wa mradi wa Mji Salama, Serikali ina mpango gani wa kuwashirikisha wananchi hasa watumishi wa umma kila mmoja angalau aweke kamera mbili za ulinzi katika eneo lake na kufanya wigo mpana wa usalama wa miji yetu.

(c) Je, kwa kuwa baadhi ya wananchi wanaoweka kamera za ulinzi wanapobaini matokeo ya uhalifu wanawajulisha Polisi kuchukuwa hatua na hatua hizo huwa hazionekani matokeo yake, je, ni lini Serikali itakaa na wadau wa ulinzi na usalama kuona kuwa ushirikiano kama huo unapatikana.

<u>Wizara ya Fedha na Mipango:</u>

118. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Kipindi kirefu sasa kumekuwa na pengo la uwepo wa sheria itakayosimamia mzunguko wote wa Bajeti kwa ujumla wake.

Kukosekana kwa sheria hiyo kunawafanya wahusika katika mzunguko wa bajeti (budget cycle), kutoonekana majukumu, mikapa na utendaji wao kwa bayana, mfano ukitolewa kwa Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi na wahusika wengine katika mzunguko.

(a) Je, kwa kuwa mabunge mengi yamekuwa na Sheria ya Bajeti inayoonesha ufanisi wa namna ya mzunguko wa Bajeti unavyofanyakazi na kusimamiwa kwa bayana, ni kwa sababu gani za msingi Sheria hiyo haitungwi kwenye Baraza letu la Wawakilishi.

(b) Je, ni lini Serikali itakaa na wadau wote katika mzunguko wa bajeti, ili kuona namna bora ya kuwa na Sheria ya Bajeti.

(c) Je, Serikali inatoa ahadi gani kwa Baraza hili la Kumi na Moja ya kuleta Mswada wa Sheria ya Bajeti ili upitishwe.

121. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliahidi kutenga kiasi cha shilingi bilioni 20 kuwalipa wateja waliokuwa wa Benki ya FBME kwa upande wa Zanzibar. Kuna taarifa kuwa BOT ilishalipa asilimia 85 kwa wadai wote Tanzania nzima na bado asilimia 15, hivyo, fedha zilizoahidiwa shilingi bilioni 20 hazijatumika bado kufanya malipo. Sambamba na hilo, wapo wafanyakazi wa FBME kwa upande wa Zanzibar ambao tokea mwaka 2017 wanahangaika kupata haki zao na wengine bado hawajapata ajira ambao wote kwa pamoja stahiki zao hazifiki hata milioni 200.

(a) Je, kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzbar ilikuwa tayari kutoa shilingi bilioni 20 kuwalipa wateja kwa upande wa Zanzibar, kwa nini haikuwatazama wafanyakazi wa benki hiyo kwa upande wa Zanzibar ambao mpaka hivi sasa hawajapata haki zao.

(b) Kwa kuwa kiwango wanachodai wafanyakazi hao ni chini ya milioni 200, ni lini Serikali itanyoosha mkono wake wa huruma na kuwasaidia wafanyakazi hao ambao wameshahangaika sana.

(c) Je, Serikali ipo tayari vipi kukutana na wafanyakazi hao na kuwasikiliza ili kuona namna ya kuwasaidia.

**Wizara ya Afya:**

219. MHESHIMIWA MMANGA MOHAMMED HAMED (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Mnyama Pweko anawaathiri sana wananchi wanaopanda mwani

katika maeneo ya bahari ya Tumbe, Micheweni, Msuka, Kiuyu na miongoni mwa madhara yake ni pale anapomwagia maji yake mtu yeyote na kumuingia, ikiwa ni pamoja na mvuvi wa mwani, mtu huyo hupoteza fahamu na kawaida hulazwa kwa siku tatu, katika hospitali ya Micheweni na Kinyasini.

Ni lini Serikali itawaekea matibabu ya dharura wananchi wa maeneo hayo, ili kuwapunguzia madhara ya mnyama pweko.

230. MHESHIMIWA MAKAME MOHAMED SUFIANI (Jimbo la Chumbuni)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Afya ya Akili imekuwa ni tatizo kubwa la dunia na kwa sasa inakadiriwa kati ya watu wanne (4), mmoja (1) ana changamoto ya Afya ya Akili. Na kati ya watu kumi (10), mmoja wao ni mgonjwa wa Afya ya Akili.

(a) Je, Serikali inaweza kueleza hali ya sasa ya Afya ya Akili ya Zanzibar, iko vipi.

(b) Je, ni wagonjwa wangapi waliobainika kuwa na changamoto ya Afya ya Akili na wanapata huduma katika Vituo vya Afya vya Serikali na Binafsi kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita.

**<u>Wizara ya Maji, Nishati na Madini:</u>**

41. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Hivi karibuni kumeshuhudiwa Kampuni ya Rand Water kutoka Afrika ya Kusini ikifanya kazi za kiutawala zilizokuwa zikifanywa na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA). Hata hivyo, ZAWA ilianzishwa kwa Sheria Namba 4 ya mwaka 2006, iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi na bado haijafutwa, licha ya majukumu yake kupewa kampuni binafsi.

(a) Je, utaratibu wa ZAWA kuipisha Rand Water kusimamia sekta ya maji, umefuata Sheria ya Maji Namba 4 ya mwaka 2006, na kama umefuata ni kifungu gani cha sheria hiyo.

(b) Kama sheria haikufuatwa, kwanini isiletwe hapa Barazani ilipotungwa na kufanyiwa marekebisho au kufutwa ili kuondoa utata wa kisheria.

(c) Je, ufanisi gani umepatikana tokea huduma za uendeshaji zihamishwe kutoka ZAWA kwenda Rand Water.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

84. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imechukuwa hatua nzuri ya kimaendeleo ya kujenga upya nyumba za maendeleo katika eneo la Kikwajuni maarufu majumba ya Mjerumani. Hata hivyo, kumekuwa na taarifa za kutatanisha kuhusu wakaazi wa eneo hilo kuhusishwa kikamilifu katika mradi huo.

(a) Je, ni kwa kiasi gani wananchi wa majumba ya Mjerumani wamehusishwa katika maamuzi ya mradi huo.

(b) Je, ni ipi hatma ya wakaazi wa majumba ya Mjerumani baada ya mradi huo kukamilika, ahadi ya Serikali kuhusu kurudishiwa makaazi yao ipo pale pale.

(c) Ni familia ngapi zitahusika na kunufaika na mradi huo.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaj, Maliasili na Mifugo:**

326. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Zanzibar imejaaliwa kuwa na misitu ya asili yenye miti ya muda mrefu na baadhi yake ina miti adimu ambayo ni rasilimali muhimu kwa uhifadhi wa mazingira na maendeleo endelevu.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhifadhi na kulinda misitu ya asili dhidi ya uharibifu.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza na kusimamia matumizi endelevu ya misitu ya asili ili kuhakikisha rasilimali hiyo inawanufaisha wananchi kwa muda mrefu.

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**

268. MHESHIMIWA SHAFI MOHAMMED SHAFI (Jimbo la Wete) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Ni jambo jema kwamba mashirika mengi ya usafirishaji ya ndani kwa njia ya anga, yameweka bei za nauli za kusafiri zinazolingana.

Hata hivyo, bei ya nauli kwa upande wa Pemba kwenda Unguja na kutoka Unguja kwenda Pemba ni tofauti na ipo juu sana.

(a) Je, ni jambo gani linalopelekea bei ya nauli kwa upande wa Pemba kwenda Unguja kuwa juu, hasa ukizingatia ni safari ya muda mfupi (nusu saa tu), tofauti na masafa ya kutoka Unguja kwenda Kilimanjaro.

(b) Je, ni lini Serikali italiingilia kati jambo hili ili wananchi wengi hasa wa Unguja na Pemba waweze kupata nafuu ya gharama ya huduma hiyo.

## Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

436. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Matukio ya kutupa watoto yamekithiri sana katika miji yetu na yamekuwa hayana muarubaini wa kuyadhibiti.

Je, hatua zipi zinastahiki kuchukuliwa dhidi ya wanawake wanaotupa watoto.

## Wizara ya Biashara na Maendelo ya Viwanda:

225. MHESHIMIWA MAKAME MOHAMED SUFIANI (Jimbo la Chumbuni)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuimarisha Biashara Ndogo Ndogo na za Kati (MSMEs) na masoko makubwa ndani na nje ya nchi.

## Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

320. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

Sekta ya TEHAMA ni nguzo muhimu ya kuharakisha maendeleo ya uchumi wa kidijitali, kuimarisha utoaji wa huduma za umma na kuongeza ajira kwa vijana kupitia ubunifu wa teknolojia.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha miundombinu ya

TEHAMA vijijini ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za kidijitali.

(b) Je, ni hatua zipi zinazochukuliwa na Serikali kwa wananchi katika kuelekea katika uchumi wa kidijitali.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

517. MHESHIMIWA ABDULLAH KAMBOTWE ABDULLAH (Jimbo la Kiembe Samaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kwa kuzingatia mchango mkubwa wa utalii katika uchumi, na kwa kuzingatia uwekezaji mkubwa uliofanywa na unaendelea kufanywa na wageni hapa Zanzibar.

(a) Je, Serikali imefanya tathmini gani ya kutambua kwa kiasi gani malipo au ankara zinazofanywa katika sekta ya utalii, zinakwenda nje ya Zanzibar.

(b) Je, Serikali imechukua juhudi gani za kisera au kisheria, katika kuhakikisha malipo na mapato yote ya utalii yanayotokana na huduma zinazotolewa hapa Zanzibar yanafanywa Zanzibar kwa manufaa ya Zanzibar.

**Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji:**

384. MHESHIMIWA DKT. MAHMOUD OMAR HAMAD (Jimbo la Tumbatu) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Ajira na Uwezeshaji:

Serikali ina mpango gani wa kutoa mikopo nafuu na masharti rahisi kwa wajasiriamali wadogo na wakati.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

264. MHESHIMIWA KHAMIS MOHAMMED AMRAN (Jimbo la Mkoani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Kutokana na mazingira ya jimbo la Mkoani kuzungukwa na bahari sehemu kubwa, wananchi wengi wa jimbo hili wanajishughulisha na uvuvi na ukulima wa mwani.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia wananchi kwa kuwapatia mitaji, ili waweze kufanya shughuli za uzalishaji kwa ufanisi.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wakulima wa mwani hapa Zanzibar hasa kisiwani Pemba ambapo mwani huzalishwa kwa wingi, ili waweze kupata bei nzuri ya mwani na kujiongezea vipato vyao.

408. MHESHIMIWA MARYAM SAID KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Serikali imekuwa na juhudi mbali mbali za kuimarisha mazingira ya biashara kwa wajasiriamali wadogo ili kujenga masoko na madiko ya kisasa yenye miundombinu bora. Lengo kuu na jitihada hizi ni kuwawezesha wajasiriamali kufanya shughuli zao katika mazingira salama, safi na yenye kuvutia ili kuongeza tija na kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja pamoja na taifa kwa jumla.

(a) Je, ni vigezo gani vilivyotumika kuwachagua na kuwaweka wajasiriamali katika masoko ya kisasa hususan katika diko la jimbo la Mkoani liliopo katika shehia ya Mbuyuni.

(b) Je, vigezo hivyo vimezingatia usawa, uwazi na mahitaji halisi ya wajasiriamali ambao walikuwepo kupisha ujenzi wa diko hilo.

<u>**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**</u>

173. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Sheria ya Utumishi wa Umma ya Zanzibar, Namba 2 ya 2011, pamoja na Kanuni zake za mwaka 2014, zimekataza wazi kwa mtumishi yeyote kujihusisha na siasa akiwa kazini. Hata hivyo, katika kipindi cha hivi karibuni, hali imeonekana kuwa tofauti hasa kwa kuongezeka watumishi wanaojinasibisha kuwa wanachama kwenye vyama vya siasa, ambao pia wanajishughulisha wazi wazi na masuala ya siasa na hutumika kupanda kwenye viriri vya mikutano au hata kutumia rasilimali za Serikali katika shughuli za siasa.

(a) Ni kwa kiasi gani Serikali inakiri kuwepo kwa tatizo hilo kwa watumishi wake.

(b) Kwa vitendo hivyo vya watumishi vinavyopelekea kupunguwa kwa imani kutoka kwa wananchi, je Serikali itachukuwa hatua gani kwa watumishi hao.

(c) Ni lini Serikali itatumia *approach* ya tathmini watendaji na

watumishi wote wa SMZ ili kuongeza ufanisi wa kazi na utoaji bora wa huduma kwa wananchi wake.

183. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Mahakama ni miongoni mwa Mihimili Mikuu katika nchi. Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 inavyoeleza Mhimili huu kuwa unapaswa kuwa huru kutekeleza kazi zake kwa usawa, uwazi na haki kwa watu wote wa Zanzibar.

(a) Kwa nini Mhimili huu mara kwa mara huwa unaingiliwa kimakusudi kupindisha baadhi ya mambo kwa maslahi ya upande mmoja.

(b) Kwa nini baadhi ya Majaji wa Mahakama Kuu hufanya kazi zilizokuwa nje ya maadili ya taaluma zao.

(c) Ni upi Mpango Mkakati wa Serikali wa kuhakikisha inawasaidia wananchi wake wa Zanzibar, kupata haki zao kupitia Mhimili huu wa Mahakama.

## II. <u>HOJA ZA SERIKALI:</u>

**<u>Waziri wa Fedha na Mipango:</u>**

Kwamba Baraza hil
i lijadili na kuukubali Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2026/2027 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2026/2027.

**Zanzibar,**
**18 Juni, 2026.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA**
**<u>WAWAKILISHI, ZANZIBAR.</u>**